*JARIDA LA CHALUFAKITA*
*Juz. 4, 2022, 80-92*

# MDHIHIRIKO WA NYUSO ZA MWANAMKE KATIKA RIWAYA YA *NYUSO ZA MWANAMKE (2010)* YA SAID AHMED MOHAMMED

Stella Faustine
Chuo Kikuu cha Dodoma-Tanzania
stelafau@gmail.com

*DOI: https://dx.doi.org/10.4314/jclfkt.v4i1.6*

**Ikisiri**

*Said Ahmed Mohammed ni miongoni mwa waandishi nguli katika fasihi ya Kiswahili. Katika kazi zake, anazungumzia masuala mbalimbali ya kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni. Kwa upande wa utamaduni, anajichomoza kama mtetezi wa wanawake kwa kuonesha madhila mbalimbali anayokumbana nayo katika jamii. Katika riwaya ya Nyuso za Mwanamke, anatumia dhana ya nyuso kama kibainishi cha namna mwanamke anavyoonekana katika jamii. Aidha, shabaha ya makala hii ni kudhihirisha namna mbalimbali za mwonekano wa mwanamke kama inavyojitokeza ndani ya riwaya hiyo. Uchunguzi na mjadala uliongozwa na Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika. Data zilipatikana maktabani kwa kutumia mbinu ya uchanganuzi matini; kisha zilichambuliwa na kuwasilishwa kwa kutumia mkabala wa kitaamuli. Matokeo ya utafiti yamedhihirisha kuwapo kwa nyuso mbalimbali za mwanamke ambazo zinajitokeza ndani ya riwaya ya Nyuso za Mwanamke kama kibainishi cha namna mwanamke anavyoonekana katika jamii. Nazo ni uwezo katika kufanya uamuzi sahihi, uwezo wa kuongoza, pamoja na uwezo wa kiuchumi.*

## 1.0 Utangulizi

Makala hii inajadili nyuso mbalimbali za mwanamke zinazodhihirika katika riwaya teule. Ili kurahisisha uelewa, tunaanza kufafanua dhana muhimu mbili, nyuso na mwanamke. BAKIZA (2010), wanafafanua dhana ya uso katika namna mbili. Kwanza, wanaeleza kuwa uso ni sehemu ya mbele ya kichwa yenye macho, pua na mdomo. Namna ya pili wanaeleza kuwa uso ni sehemu ya mbele ya gari au ya juu kwenye kitu kama vile ubao. Ufafanuzi huu unashabihiana na ule wa BAKITA (2017), ambao pia wanafafanua dhana hii kuwa; Kwanza, uso ni sehemu ya mbele ya kichwa cha binadamu au mnyama ambapo macho, pua, mdomo kidevu na paji hupatikana. Pili, ni sehemu ya nje au ya juu ya kitu kama kinavyoonekana kwa macho na huweza kugusika. Wingi wa uso ni nyuso. Kutokana na fasili zilizotolewa, kwa muktadha wa makala hii, dhana ya nyuso inatumika kumaanisha namna mbalimbali za mwonekano ambao mtu anaweza kuwa nazo. Mwanamke ni mtu mwenye jinsia ya kike (BAKIZA, 2010). Hivyo,

katika makala hii tunapojadili mdhihiriko wa nyuso za mwanamke, tunalenga kubainisha namna mbalimbali za mwonekano wa mwanamke kwa kadri anavyotazamwa na jamii kwa kuzingatia mifano kutoka riwaya ya *Nyuso za Mwanamke*.

Katika mtazamo wa kiulimwengu, kwa miaka mingi sasa mwanamke amekuwa akichukuliwa kama kiumbe dhaifu katika jamii. Hii inatokana na mifumo mbalimbali inayolenga kumdidimiza kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni. Hali hii imesababisha kupuuzwa kwa haki za wanawake kama viumbe kamili (Njogu na Chimerah, 1999).

Licha ya hatua mbalimbali zinazochukuliwa kumkweza mwanamke kama inavyoelezwa na Gibbe (1993), Sawe (2018), Mwinyi (2020) na Faustine (2022) ambao wanabainisha 'mtazamo-sasa' wa jamii kuhusu mwanamke, kwa kiasi kikubwa, kwa Waafrika, nafasi ya mwanamke bado imekuwa ikiwekwa kwenye daraja la chini. Waafrika wanamtazama mwanamke kama mtu dhaifu asiyeweza jambo lolote. Hivyo, uwezo wa mwanamke katika suala la uamuzi, utendaji au utekelezaji wa mambo mbalimbali umekuwa ukiwekwa chini ya uangalizi wa mwanamume. Hili linathibitishwa na wataalamu mbalimbali; miongoni mwao ni Balisidya (1982), Omari (2011) na Masele (2012). Kwa ujumla, wataalamu hawa wanahitimisha kuwa bado mwanamke amekuwa akitazamwa kama chombo au daraja la kuwezesha kuikamilisha safari ya mwanamume.

Unyanyasaji wa kijinsia dhidi ya wanawake unaotokana na itikadi mbalimbali za kijamii ndio uliozua vuguvugu la harakati za kifeministi zilizolenga kupambana na mfumo unaomkandamiza mwanamke. Wafula na Njogu (2007) wanatuambia kuwa, kinadharia, harakati za ufeministi zilianza kuzungumziwa katika karne ya kumi na tisa na kushamiri zaidi kati ya miaka ya 1960 hadi 1970. Katika kipindi hiki, wanawake wa mataifa ya Kimagharibi walianza kuzungumza juu ya matatizo yao katika machapisho mbalimbali. Kazi mbalimbali ziliandikwa zikiwa na mwelekeo wa kusaili nafasi ya mwanamke pamoja na kudai haki ya kufanya uamuzi katika jamii. Miongoni mwazo ni insha ya *A Room of One's Own* (1929) ya Virginia Woolf. Nyingine ni vitabu vya *A Vindication of the Rights of Women: With Structures on Moral and Political Subjects* (1792) ya Mary Wollstonecraft pamoja na *The Second Sex* (1949) ya Simone de Beauvoir.

Kwa upande wa Afrika, vuguvugu hili halikuwaacha nyuma waandishi wa fasihi ya Kiswahili. Walitumia kalamu zao kuonesha madhila mbalimbali anayokumbana nayo mwanamke katika jamii za mfumo dume uliokumbatiwa kwa mwamvuli wa mila na desturi. Baadhi ya kazi zilizoandikwa kwa kubainisha matatizo mbalimbali anayokumbana nayo mwanamke kutokana na mfumo huo ni *Utengano* (1980), *Tata za Asumini* (1990), *Vuta N'kuvute* (1999), *Kasri la Mwinyi Fuadi* (2007) na *Nyota* (2022).

Pamoja na changamoto anazokumbana nazo mwanamke zinazomfanya kuonekana kama kiumbe duni, jamii pia haikuacha kumtazama kwa upande chanya. Jambo hili linathibitishwa na wataalamu mbalimbali wa fasihi. Miongoni mwao ni Songoyi (2005) ambaye anafafanua kuwa, katika jamii ya Wasukuma, mwanamke hupewa heshima ya kuthaminiwa kama mlezi wa ukoo kutokana na majina yao, pamoja na majina ya koo zao kurejelewa kwa kutumia majina ya wanawake. Perry (2007) anatoa mtazamo sawa na uliotolewa na Songoyi (khj) kwa kufafanua kuwa, licha ya mwanamke kutazamwa kama kiumbe dhaifu, katika jamii ya Wasukuma kuwapo kwa mwanamke katika kaya ni kiashiria cha ustawi wa kaya hiyo. Hii ina maana kuwa pasipo mwanamke hakuna kaya, hivyo mwanamke ni kiini cha kaya. Aidha, Faustine (2022) anaonesha namna *Utenzi wa Mwana Kupona* unavyobainisha majukumu mazito anayokabiliana nayo mwanamke kama kiongozi na msimamizi wa familia. Hii ni kinyume na mitazamo ya wataalamu wengine kama vile Mwachofi (1987) na Momanyi (2007) ambao wanadai kuwa utenzi huo ni kielelezo cha kumdhalilisha mwanamke.

Kwa jumla, mwonekano wa mwanamke katika jamii ambao unakitwa katika u-hasi na u-chanya, kama inavyojadiliwa na wahakiki na watafiti wa kazi za fasihi, ndio ulioleta msukumo wa kufanyika kwa utafiti uliozaa makala hii. Shabaha ni kubainisha udhihirikaji wa nyuso za mwanamke ambazo zinajitokeza ndani ya riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* kama kibainishi cha namna mwanamke anavyoonekana katika jamii.

## 2.0 Kiunzi cha Nadharia

Utafiti uliozalisha makala hii uliongozwa na misingi ya Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika. Nadharia hii hushughulikia maswala ya kijinsia kwa kujikita katika muktadha wa Kiafrika. Mwasisi wa nadharia hii ni Steady (1981). Mwananadharia huyu anaamini kuwa dhuluma ambazo zimekuwa zikimgandamiza mwanamke zinatokana na misingi iliyowekwa na asasi mbalimbali za kijamii; hivyo, kumnyima haki zake za msingi. Steady (1981) anafafanua kuwa Ufeministi wa Kiafrika huweka pamoja maswala ya kijinsia, ubaguzi, utabaka na mielekeo tofauti ya kiutamaduni ili kuibua Ufeministi unaomwangalia mwanamke kama kiumbe kamili.

Ifuatayo ni misingi ya Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika kwa mujibu wa Steady (1981): Mosi, Kutoa msukumo katika ukombozi wa mwanamke kutokana na pingu zilizowekwa na mifumo ya kijamii. Miongoni mwa mifumo hiyo ni asasi za kitamaduni kama vile mila na desturi, ndoa na dini. Wanaufeministi wa Kiafrika wanaamini kuwa asasi hizi zimejengwa kwenye imani na uwezo mkubwa alionao mwanaume na kuishia kumwangalia mwanamke kama chombo tu. Zinatilia mkazo itikadi za kiume zinazopatikana katika jamii na kuishia kuzipa nguvu tamaduni dhalili dhidi ya mwanamke. Hivyo, Wanaufeministi wa Kiafrika hukusudia

kupinga na kutupilia mbali misingi inayojengwa na asasi hizo ili kufanikisha malengo ya ukombozi wa mwanamke. Pili, kutafsiri uzoefu na tajriba za wanawake kama zinavyojitokeza katika tanzu mbalimbali za fasihi. Unashambulia pia mitazamo ya kiume kuhusu wanawake wanavyopaswa kuhisi, kufikiri na kuitikia hali mbalimbali za maisha. Tatu, Ufeministi wa Kiafrika unalenga kuamsha na kuzindua mwamko miongoni mwa wanawake ili wawe watendaji zaidi na washiriki ipasavyo katika ukombozi wao wenyewe. Nne, Ufeministi wa Kiafrika unasisitiza umuhimu wa kuvumbua na kuweka wazi kazi za sanaa zilizotungwa na wanawake ambazo zimepuuzwa kwa sababu ya utamaduni unaompendelea mwanamume. Tano, unajaribu kuhamasisha utungaji wa kazi za sanaa zenye wahusika wa kike wanaoweza kuigwa, wanawake ambao hawawategemei wanaume ili wajitambulishe.

Nadharia hii ilisaidia katika ukusanyaji na uchanganuzi wa data kwa namna ifuatayo: Mosi, kubaini namna asasi mbalimbali za kijamii kama ndoa, utamaduni na dini zinavyotumika kumkandamiza mwanamke kwa kuhusisha maudhui yanayowasilishwa ndani ya riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* na hali halisi ya maisha ya jamii husika. Pili, ilimwongoza mtafiti kubaini namna mwandishi anavyomuwasilisha mhusika mwanamke kama binadamu kielelezo na sio binadamu linganishi katika harakati zake za kusaka uhuru wake ili atambuliwe kama binadamu kamili katika jamii. Tatu, ilisaidia kutoa miongozo ili kubaini jitihada mbalimbali anazofanya mwanamke ili kujikwamua na minyororo ya kitamaduni inayomkandamiza na kumfanya aonekane kuwa ni kiumbe dhaifu.

## 3.0 Methodolojia ya Utafiti

Utafiti uliozalisha makala hii umefanywa kwa kuzingatia mkabala wa kitaamuli. Data za utafiti zilikusanywa maktabani kwa kutumia mbinu ya uchanganuzi wa matini. Mbinu hii humpa mtafiti undani wa masuala yanayotafitiwa kwa kuyalinganisha na ama kuyapatanisha na ushahidi kutoka katika vyanzo vya awali (Ponera, 2019). Kwa kuzingatia mbinu hii, data za utafiti ziliegemezwa katika makundi mawili ambayo ni data za msingi na data za upili. Data za msingi zilipatikana katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* ya Said Ahmed Mohamed (2010). Riwaya hii ilipatikana kwa kutumia mbinu ya usampulishaji lengwa kutokana na maudhui yake kushabihiana kwa kiasi kikubwa na mada tafitiwa pamoja na shabaha ya utafiti. Data za upili zilipatikana maktabani kutoka katika vyanzo mbalimbali vya maarifa kama vile vitabu, majarida na tasinifu mbalimbali ambazo maudhui yake yanashabihiana na mada husika.

## 4.0 Mjadala wa Matokeo ya Utafiti

Sehemu hii inahusu mjadala wa matokeo ya utafiti. Nayo imegawanyika katika vijisehemu muhimu viwili. Navyo ni muhutasari wa riwaya teule, pamoja na

mjadala kuhusu udhihirikaji wa nyuso za mwanamke katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke*.

### 4.1 Muhutasari wa Riwaya ya *Nyuso za Mwanamke*

*Nyuso za Mwanamke* ni riwaya iliyoandikwa na Said Ahmed Mohammed na kuchapishwa mwaka 2010 na Longhorn Publishers, Nairobi. Katika makala hii, toleo lililotumika katika upatikanaji wa data za utafiti uliozalisha makala hii ni la mwaka 2010. Riwaya hii ina jumla ya sura thelathini (30) ambazo zinajadili, kuchimba na kuchambua matatizo mbalimbali yanayomkabili mwanamke katika jamii; kiutamaduni, kiuchumi na kisiasa.

Katika riwaya hiyo tunatambulishwa mhusika Nana, binti ambaye analelewa chini ya uangalizi wa baba yake na mama wa kambo. Hii inatokana na sababu kuwa mama yake Nana, Bimkubwa alitengana na baba yake miaka mingi iliyopita na baadaye kufariki. Nana anabainisha wazi upweke alionao kwa kumkosa mama yake pale anapolalamika kwa kujisemea peke yake kuwa hajui kama mama yake anayahisi maumivu aliyonayo ndani ya moyo wake. Maumivu aliyoyapata na kuishi nayo toka alipomuhitaji tangu akiwa mtoto mpaka ukubwani. Nana analalamika kwa kusema kuwa maumivu na uchungu wa akili alionao kwa kumkosa mama yake, yamemzuia kuvunja ungo (uk. 19).

Hata hivyo, Nana anapotimiza umri wa miaka ishirini na moja anavunja ungo. Baba yake anamuandalia sherehe iliyolenga kumfundisha misingi ya yeye kuwa mwanamke. Ingawa Nana anakataa sherehe hiyo kwa vile iliegemea zaidi maslahi ya mwanaume, baba yake na mama wa kambo wanamlazimisha kuhudhuria. Anasema: “sherehe ya leo ililazimishwa kama zilivyolazimishwa sherehe zangu zote. Hasa kwa vile ilichanganywa na kuwa kwangu mtu mzima…” (uk. 32). Wakati wa sherehe hiyo, Nana anatambulishwa kwa mchumba asiyemtaka aitwaye Dusa. Nana anamkataa kwani hakumchagua yeye bali amechaguliwa (uk. 44). Hii ni kwa sababu Nana hakuamini katika harusi ya kushurutishwa bali iliyojengwa katika misingi ya maelewano (uk. 233).

Malezi ya baba na mama wa kambo hayamridhishi Nana. Maisha ya kulindwa, kuchungwa kwa kisingizio cha kwamba yeye ni mtoto wa kike hayakumfurahisha. Anaamua kupingana na utumwa huo, anakataa kupelekwa shuleni na kurudishwa kwa gari kwani yeye si mtoto mchanga tena. Anahitaji kujifunza kuwa peke yake na dunia yake. Hata hivyo, baba yake anakataa na kumwambia Nana kuwa bado ni mwanagenzi wa dunia, na tena ni mwanamke na hivyo lazima amlinde (uk. 38). Pamoja na malezi mazuri anayoyapata, Nana ananyimwa uhuru wa kuwa na mamlaka ya kuamua jambo lolote analolitaka kwa utashi wake. Anaamua kutoroka nyumbani kwao. Kinyume na matarajio yake, jamii nayo inampokea kwa makucha yaleyale ya kumweka utumwani. Kila anakojaribu kupita anakutana na vikwazo vinavyomtaka kutii sheria na matakwa ya mwanaume ili aweze kufanikiwa. Hata

hivyo, licha ya misukosuko mingi anayoipata, Nana anafanikiwa kuvunja minyororo inayomweka utumwani. Anapojitazama katika kioo na kujiona ana nyuso nyingi, anaamua kuianza safari mpya ya maisha yake yenye uhuru kamili.

### 4.2 Mdhihiriko wa Nyuso za Mwanamke katika Riwaya Teule

Katika riwaya ya Nyuso za Mwanamke, Said Ahmed Mohamed anatumia dhana ya ‘Nyuso za Mwanamke’ kama kibainishi cha namna mwanamke anavyoonekana katika jamii. Utafiti wetu umebainisha nyuso tatu tofauti ambazo zinajitokeza ndani ya riwaya hiyo. Nazo ni uwezo katika kufanya uamuzi sahihi, uwezo wa kuongoza, pamoja na uwezo wa mwanamke kiuchumi.

#### 4.2.1 Uwezo katika Kufanya Uamuzi

Katika kipengele hiki, uso wa mwanamke katika kufanya uamuzi umetazamwa katika pande mbili. Upande wa kwanza ni hasi ambao unamwangalia mwanamke kama kiumbe dhaifu ambaye hana hiyari ya kufanya uamuzi. Upande wa pili ni chanya. Hapa mwanamke anaangaliwa kama kiumbe jasiri mwenye uwezo wa kufanya uamuzi kulingana na matakwa binafsi au ya jamii.

Tukianza na upande hasi, jamii nyingi duniani, hasa zinazofuata mfumo dume, mwanamke amekuwa akitazamwa kama kiumbe duni asiyekuwa na uwezo wa kufanya uamuzi. Nafasi yake imekuwa ikiwekwa katika ufinyu wa kimawanda tofauti na anavyotazamwa mwanaume (Mbughuni, 1982). Kwa Waafrika, ambako jamii nyingi zinatawaliwa na mfumo dume, uwezo wa kufanya uamuzi kwa jinsi ya kike umekuwa ukiminywa katika maeneo mbalimbali. Miongoni mwayo ni masuala ya ndoa ambazo kwa kiasi kikubwa zinafungamanishwa na matakwa ya mila, desturi, itikadi pamoja na falsafa inayotawala maisha yao. Waafrika wanaamini kuwa mwanamke au binti aliyefikia umri wa kuolewa hana uwezo mzuri wa kiutambuzi kati ya jema na baya. Maisha yake yamekitwa katika misingi ya kuongozwa na kuchaguliwa lililo zuri na kuepushwa na baya. Katika muktadha unaofumbatwa na itikadi pamoja na mila na desturi za Mwafrika, hiyari ya mtoto wa kike ni kukubaliana na uamuzi unaofanywa na wazazi wake au unaotokana na jamii na si vinginevyo. Hapa ndipo huvikwa uso kama kiumbe dhaifu asiyeweza kufanya uamuzi sahihi kwani hana hiyari ya kufanya uamuzi kulingana na utashi wake.

Wanaufeministi wa Kiafrika wanaamini kuwa ndoa kama asasi mojawapo ya utamaduni ina mchango mkubwa katika kumdhalilisha mwanamke, hasa kutokana na pingu inazomtia utumwani; hivyo, kumnyima uhuru wa kufanya uamuzi binafsi. Hapa mwanamke anatakiwa awe mtii na kukubaliana na kila linaloamuliwa na wazazi au jamii yake. Katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* uso wa mwanamke kama kiumbe asiyeweza kufanya uamuzi binafsi unadhihirika pale mwandishi anapoonesha madhila mbalimbali wanayokumbana nayo wanawake kwa kuchaguliwa wenza na wazazi ili kukidhi matakwa ya jamii na hulazimika

kutii, kwani hana uwezo wa kufanya uamuzi kulingana na misingi ya jamii. Mfano mzuri ni mhusika Bi. Mkubwa (mama yake Nana), anayechaguliwa mume wa kuishi naye. Kwa kuhofia kukiuka matakwa ya wazazi wake, anaamua kuolewa bila kuwa na mapenzi na yule aliyemuoa. Haya yanabainishwa na Nana pale anaposema kuwa: "Mimi sitataka kuchaguliwa kama alivyochaguliwa mama'angu" (uk. 42.).

Mhusika mwingine anayeangaliwa kama kiumbe asiyeweza kufanya uamuzi binafsi ni Shemsa. Anatii kila jambo analoamuliwa na wazazi wake. Hii inatokana na mifumo ya jamii aliyomo ambayo imemlea na kumkuza. Ingawa hakutaka kuolewa na Sadiki mchumba aliyechaguliwa na wazazi wake, minyororo ya desturi inamfunga na kumlazimisha kutii sheria na mamlaka kama anavyotueleza Bi. Kivumbasi:

> …hapa petu mwanamke haposi, huposwa; na anapoposwa akikataa huwa jambo kubwa ikiwa familia yake wanataka binti yao aolewe na huyo mwanaume aliyekuja kuposa. Basi kinyume cha mambo, huwa mwanaume wanayemtaka wao siye anayemtaka binti yao. Ikiwa binti yao atamkataa mwanaume wanayemtaka wao, basi wazee watatumia kila hila, na hila zikishindwa nguvu, na iwapo nguvu hazikufanya kazi, hutumia msusio… hapa petu, mwanamke hawezi kumkataa mwanamume anayemposa hata kama hamtaki (uk. 208).

Utiifu na unyenyekevu anaojengewa mwanamke hauishii katika masuala ya mahusiano ya ndoa peke yake. Mwandishi anatuonesha kuwa uamuzi wowote katika jamii zinazotawaliwa na mfumo dume uko chini ya mamlaka ya mwanaume. Katika muktadha huu, mwanamke hubaki kuitikia hewala kwa kila analoamuliwa. Hana nafasi ya kutoa ushauri wowote katika jamii hata ikiwa anahusika moja kwa moja na suala linalohitaji ufumbuzi. Siku zote amekuwa mnyenyekevu kwa kutaka suluhu na salama yake anayoipata ndani ya utii uliojengwa na wigo wa jamii. Jambo hili linajibainisha katika kisa cha Bi. Mau anaposimulia namna mke alivyompa ushauri mumewe wa kutomwozesha binti yake kwa mume asiyemtaka. Matokeo yake, mume alimuona mkewe kuwa mpumbavu kwa ushauri wake (uk. 69).

Uso mwingine unaodhihirika katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* ni ule unaomwonesha mwanamke kwa mtazamo chanya kama mtu mwenye uwezo wa kufanya uamuzi. Hii inabainika kupitia wahusika Bi. Mkubwa na Shemsa ambao kutokana na misingi ya jamii yenye mfumo dume wanafungwa katika minyororo ya ndoa ya kulazimishwa. Hata hivyo, matakwa binafsi ya kujiweka huru yanayochochewa na mabadiliko ya kimazingira na msukumo wa kiwakati yanasababisha wahusika hawa kusimama kama wanawake wenye uwezo wa kufanya uamuzi bila kuyumbishwa. Wanaamua kuachana na ndoa zao ili kuutafuta uhuru wao uliominywa kwa kulazimishwa kuolewa na wanaume wasiowapenda.

Shemsa anadhihirisha hili pale anapoamua kudai talaka. Anasema: "Ilinibidi nidai talaka hata wazee wangu wangeniachia radhi namna gani" (uk. 211).

Pia, uamuzi wa Nana wa kupinga sheria za kuamuliwa na yeye kutii unadhihirisha uso wa mwanamke kama kiumbe mwenye uwezo wa kufanya uamuzi binafsi. Wanaufeministi wa Kiafrika wanaamini kuwa ukombozi wa mwanamke utaletwa na mwanamke mwenyewe pale atakapozinduka, kushiriki, na kuwa mtendaji katika ukombozi wake mwenyewe. Katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke*, tunamuona Nana akisukumwa na utashi na matakwa binafsi kupinga sheria zinazombana na kumfanya aishi kama mtumwa. Hajali jamii yake itamchukuliaje. Kama ambavyo Wanaufeministi wa Kiafrika wanamini kuwa ndoa ni asasi mojawapo inayochangia kumdidimiza mwanamke, Nana anaamua kususia ndoa na kwenda kinyume na matakwa ya baba yake. Kutokana na msukumo wa kiwakati na mabadiliko ya jamii, shauri kubwa analolisimamia ni uhuru wake binafsi. Katika kuusimamia uhuru huo, anaanza kwa kukataa kuchaguliwa mchumba. Anasema:

> …Mimi nilimkataa katakata Dusa awe mwenzi wangu wa kuishi nami milele. Wa kulala naye kitanda kimoja. Dusa ni kijana mwenzangu ndiyo lakini sikumchagua. Nimechaguliwa na babangu awe mchumba wangu na hatimaye mume wangu (uk. 44).

Kisha, anakataa kuchungwa na kuandamwa na walinzi kwa kumpeleka shule kila siku na kufuatwa. Nana anapinga hili kwa kusema:

> … nilikataa kupelekwa shule na kurudishwa kwa gari. Nilikataa tu na kumwambia baba kwamba mimi si mtoto mchanga tena. Nilikuwa nataka kuwa peke yangu na dunia yangu. Baba alikasirika sana. Akanambia wazi kwamba bado mimi ni mwanagenzi wa dunia. Tena mimi ni mwanamke (uk. 38).

Nana anaendelea kuonesha kiu ya kuusaka uhuru wake kwa kusema:

> … Alitishia kuninyima haki zangu za ubinti, lakini mimi nilishika uzi huohuo wa kutotaka kupelekwa shule na kurudishwa kwa gari. Nilihisi kwamba haki ya kuwa huru ni haki yangu ya kwanza ya msingi. Nilikataa katakata kuchukuliwa kwa gari, kwa hiyo niligoma kwenda shule. Mpaka baba alipoona si mchezo tena, ndipo alipoamuru niende shule kwa gari, lakini nirudi kwa miguu (uk. 39).

Kiu ya kuusaka uhuru inamfanya Nana kuchukua uamuzi mgumu. Haishii tu kupinga yale anayoamuliwa na wazazi wake, bali anaamua kuondoka nyumbani kwao na kuutafuta uhuru binafsi. Uamuzi huu unaonesha uso mwingine wa mwanamke kama mtu mwenye uamuzi chanya, unaokaidi misingi ya jamii yenye

mfumo dume. Nana anakiri uamuzi wa kuikimbia hali yake ya uanamke iliyofumbatwa na misingi ya ujadi. Anakataa uhasi aliojengewa kama mwanamke kwa maana yao (wanaume na misingi ya utamaduni wa jamii) na kujivika mtazamo mpya wa usawa wa kuwa kama wao (wanaume). Huu ni ule unaojengwa katika maana ya kuwa na uamuzi na uhuru wa kujiamulia kutenda jambo. Uhuru ambao Wanaufenisti wa Kiafrika wanadai kuwa umekuwa ukiporwa na misingi ya tamaduni mbalimbali za kijadi kwa muda mrefu, hivyo kumfunga mwanamke katika minyororo ya utumwa. Wamitila (2003) anaeleza kuwa mielekeo ya kiutamaduni katika jamii ni chachu ya ukandamizwaji wa mwanamke, kwani humfanya mwanamume kama kaida au binadamu-kielelezo na kuishia kumwangalia mwanamke katika misingi ya kiulinganishi tu. Wanaufeministi wa Kiafrika wanamini kuwa utamaduni anamokulia mwanamke ndio unaomjenga na kumfanya kuamini kuwa anapaswa kuikubali hali aliyomo. Mtazamo huu umekusudiwa kuzipinga tamaduni zinazomgandamiza mwanamke na kuleta usawa baina ya wanawake na wanaume katika jamii.

Kwa jumla, kupitia wahusika waliodondolewa mwandishi amefanikiwa kuudhihirisha uso mmojawapo wa mwanamke kuwa ni kiumbe mwenye uwezo wa kufanya uamuzi sahihi kwa mustakabali wa ridhiko la moyo wake na maisha yake kwa ujumla.

### 4.2.2 Uwezo wa Kuongoza

Kama zilivyo jamii nyingine duniani, jamii za Kiafrika pia huzingatia mgawanyo wa majukumu kwa kuangalia jinsi baina ya wanawake na wanaume. Suala la uongozi huzingatia mfumo huo, ambapo mwanamke hutazamwa kama kiumbe asiyeweza kuiongoza jamii (Haji, 2014). Nafasi yake huwekwa katika kiwango cha familia ambapo hupewa jukumu la uzazi na ulezi wa familia. Haji (khj) anaeleza kuwa katika jamii zenye mfumo dume, hususani jamii nyingi za Kiafrika, mtoto wa kiume huandaliwa kuwa shujaa na kushika nafasi za uongozi, huku mtoto wa kike akiandaliwa kuwa mama na mlezi wa familia. Katika mtazamo huu, waandishi wa kazi za fasihi wamekuwa wakimsawiri mwanamke kama kiumbe duni kwa kumuweka katika daraja la chini. Hii ni pamoja na kumpa majukumu ambayo yanaonekana kuwa mepesi na ya mawanda ya familia. Katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke*, Nana anabainisha hili kwa kusema:

> … maisha yetu wanawake hapa petu yamefinyangwa ndani ya tamaduni zilizoasisiwa na mwanamme ambazo bado zina nguvu kubwa kupita kiasi. Zinafanana na tamaduni za *the untouchable* ambamo waliozaliwa vinyozi wanabaki kuwa vinyozi mpaka wajikekete nyembe na kujimaliza wao wenyewe; wanaokuja duniani wapishi, wapike bondo maisha yao yote, mpaka moshi uwasonge kooni kuwaziba pumzi wao wenyewe; wanaotokana na koo za wakulima wainue na kushusha majembe siku zote … (uk.107).

Kimsingi, nukuu hii inabainisha majukumu ambayo kwa kadri ya mitazamo ya jamii za Waafrika au jamii zinazofuata mfumo dume humdidimiza mwanamke na kumfanya aonekane kuwa kiumbe duni.

Hata hivyo, pamoja na mifumo ya kijamii kumweka mwanamke katika daraja la chini, katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke*, tunaona uso mwingine wa mwanamke pale anapojinyumbua katika mtazamo chanya kama kiongozi mwenye uwezo mkubwa wa kuongoza. Kama ambavyo Wanaufeministi wa Kiafrika wanaamini kuwa ukombozi wa mwanamke uko mikonomi mwa mwanamke mwenyewe (kupitia kuipinga mifumo mbalimbali ya kijamii inayomgandamiza), katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* tunaoneshwa namna Bi. Chuma anavyoamua kutupilia mbali mtazamo wa ubabedume kuwa kiongozi wa familia ni mwanamume. Mhusika huyu anaamua kutekeleza majukumu mbalimbali ya familia pasipo kutetereka, tofauti na mipaka aliyowekewa na jamii. Mwandishi anatueleza ujasiri na ushupavu wake katika kuiongoza familia yake kwa kusema:

> …Na yeye, kusema kweli, amechoka kukaa katika nyumba hii ya pamoja inayoongozwa na Bi Chuma, yule mwanamke shupavu, shujaa na mwerevu. Na kwa upande wake yeye alichoka kuona dunia yake inaongozwa na Faisal (uk. 158).

Vilevile, mwandishi anaonesha uimara wa mwanamke katika uongozi kwa kumtumia Nana. Licha ya kupita katika mkondo wa maisha uliomwegemeza katika uongozi wa mwanaume, anaamua kuikata minyororo na kuupa nafasi wakati. Kwanza, anajikubali yeye kama mwanamke; kisha anasimama kama kiongozi mwenye uwezo wa kujiongoza na kuwaongoza walioko chini yake. Hii inadhihirika pale mwandishi anapoeleza namna Nana anavyomudu kuwa na ofisi yake, huku yeye akiwa mkurugenzi na kuwaongoza waendeshaji wa ofisi yake. Mwandishi anatueleza hivi:

> Ghorofa ya tatu na ya nne pana ofisi zote za utawala wa miradi yake Nana, ikiwemo ofisi yake yeye mwenyewe, Mkurugenzi na ya msaidizi—mshauri wake Faisal. Bila ya shaka ofisi hizo zina masekretari, na makarani, wahasibu, mshikafedha na wasaidizi wake na mwendesha ofisi na wasaidizi wake (uk. 197).

Kimsingi, katika jamii za mfumo dume, mwanamke anatazamiwa kuwa mtu wa kuongozwa na si kuongoza watu wengine, hususani wanaume. Kitendo cha mwanamke kutupilia mbali misingi ya mfumo dume na kusimama kama kiongozi kinabainisha uso mwingine wa mwanamke—kuwa, kwa upande mmoja, ni kiumbe anayeweza kuongozwa na kutii kulingana na matakwa ya jamii; na, kwa upande mwingine, ni kiumbe anayeweza kusimama na kuongoza kama wafanyavyo wanaume pasipo kutetereka.

### 4.2.3 Uwezo wa Kiuchumi

Katika jamii, mwanamke amekuwa akitazamwa kama kiumbe tegemezi anayetakiwa kuhudumiwa na si kuchangia katika huduma wala yeye kuhudumia. Kwa mujibu wa Wana ufeministi wa Kiafrika, mtazamo huu umekuwa ukirudisha nyuma maendeleo ya jamii, kwani kutokana na mfumo unaowekwa, mwanamke amekuwa akipewa nafasi finyu katika kuchangia maendeleo hayo (Kitundu, 2012). Mtazamo huu ambao unaujenga uso wa mwanamke katika utegemezi umesawiriwa katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke*. Mwandishi anaonesha hili pale Nana anapomwelezea mama yake wa kambo kama mwanamke tegemezi anayetegemea kufanyiwa kila kitu na mumewe pasipo yeye kujishughulisha. Anasema:

> Mimi (nisikilize vizuri), licha ya kutotaka kubaki jikoni kupika na kupakua, kuosha vyombo na kufagia na kutunza watoto, sitaki mimi kamwe hata kuwa mwanamke kwa maana ya mwanamke anayetunzwa na kulindwa na mwanamume kama mamangu wa kambo au mwanamke hohehahe anayefonzwa damu taratibu, huku akimalizika kama alivyomalizika mamangu mzazi (uk. 109).

Hamu ya kujitegemea inamfanya aikwepe hata misaada mbalimbali ambayo ingemfanya kuwa tegemezi kwa namna moja au nyingine. Kwa uamuzi huu, anakata shauri la kutopokea msaada wowote kutoka kwa Faisal ili kuweza kuusimamisha muziki wake wa taarabu. Kama mwanamke, anatumia uwezo wake wa akili na kusimama. Hata pale muziki wa taarabu unapopigwa vita na kuonekana ni haramu kuimbwa na mwanamke, anasimama imara kupigana vita ya kiuchumi inayoweka mipaka baina ya mwanamke na mwanamume. Imani, uwezo wa kufanya uamuzi, na uthubutu vinamfanya Nana asimame imara na kuishinda vita hiyo. Anaanzisha kampuni yake ambayo inamwezesha kiuchumi pamoja na kuajiri watu wa marika mbalimbali (uk. 197).

## 4.0 Hitimisho

Makala hii imebainisha nyuso mbalimbali za mwanamke zinazodhihirika katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke*. Nyuso zilizobainika katika utafiti na kuwasilishwa humu ni: uwezo wa kufanya uamuzi sahihi, uwezo wa kuongoza, pamoja na uwezo wa kiuchumi. Kupitia nyuso hizo, makala imebainisha kuwa mwanamke hawezi kutazamwa katika upande mmoja wa uhasi kama misingi ya jamii inavyomjenga kuwa, bali huweza kujinyumbua katika nyuso tofauti. Kwa jumla, kama ambavyo imefafanuliwa katika vipengele hivyo, *Nyuso za Mwanamke* ni riwaya ambayo inaonesha uwili wa kimtazamo wa mwanamke kwa kadri anavyoweza kujinyumbua kutokana na msukumo wa mabadiliko ya kijamii, kiwakati na kimazingira.

**Marejeleo**


Balisidya, M. L. (1982). The Image of Woman in Tanzania Oral Literature. *Kiswahili*, 49(2), 1-31.

BAKITA, (2017). *Kamusi Kuu ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers Limited.

BAKIZA, (2010), *Kamusi la Kiswahili Fasaha*. Nairobi: Oxford University Press.

Beauvoir, S. (1949). *The Second Sex.* Harmondsworth: Penguin.

Faustine, S. (2022). *Utenzi wa Mwana Kupona*: Kilingo cha Utwezaji wa Mwanamume? *Nuru ya Kiswahili*, 1(1), 119-137.

Faustine, S. (2022). *Nyota.* Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers Ltd.

Gibbe, A. (1993). Women and the Making of Literature in East Africa. OSSREA 4th Issue Competition. Muswada.

Haji, H. I. (2014). *Usawiri wa Mwanamke katika Riwaya za Shafi Adamu Shafi*. Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dodoma.

Khamis, S. A. M. (2010). *Nyuso za Mwanamke*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Kitundu, N. J. (2012). *Usawiri wa Wahusika Wanawake katika Ngano za Wanyiramba.* Tasinifu ya Uzamili (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Masele, E. J. (2012*). Sukuma Women and Men's Songs: A Comparative Study*. MA Dissertation (Not Published), University of Dodoma.

Mbughuni, P. (1982). The Image of Woman in Kiswahili Prose Fiction. *Kiswahili*, 49(1) 15 – 24.

Momanyi, C. (2007). Patriarchal Symbolic Order: The Syllables of Power as Accentuatuated in Waswahili Poetry. *The Journal of Pan African Studies*, 1(8), 18 - 23.

Mwachofi, A. (1987). *Mama Eee*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Mwinyi, Y. M. (2020). *Kilingo cha Utenzi wa Mwana Kupona katika Usawiri wa Mwanamke wa Pwani: Mifano kutoka Kisiwa cha Tumbatu na Lamu*. Tasinifu ya Shahada ya Uzamivu (Haijachapishwa), Chuo Kiku cha Dodoma.

Njogu, K. na Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyata Foundation.

Omary, S. (2011). Taswira ya Mwanamke katika Muziki wa Bongo Fleva: Mifano kutoka katika Nyimbo Teule. *Mulika*, (30), 69-83.

Perry, M. (2007). *Western Civilization. Ideas Politics, and Society*. New York: Hongkong Miffling Company.

Ponera, A. S. (2019). *Misingi ya Utafiti wa Kitaamuli na Uandishi wa Tasinifu*. Dodoma: Central Tanganyika Press.

Said, A. M. (1980). *Utengano*. Nairobi: Longman.

Said, A. M. (1990). *Tata za Asumini*. Nairobi: Longman.

Sawe, A. (2018). *Usawiri wa Mwanamke katika ndoa Mifano kutoka Utenzi wa Mwana Kupona na Utendi wa Ayubu na Matini Teule za Kidini.* Tasinifu ya Shahada ya Uzamivu (haijachapishwa), Chuo Kikuu Moi.

Shafi, A. S. (1999). *Vuta N'kuvute*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers Ltd.

Shafi, A. S. (2007). *Kasri ya Mwinyi Fuad*. Nairobi: Vide-Muwa

Steady, F.C. (1981). *Black Women Cross - Culturally*. Cambridge: Scherkman Publishing Co.

Songoyi, E. M. (2005). *The Form and Content of the Wigashe Dance Songs of the Sukuma*. Phd Disertation (not Published), University of Dar es Salaam.

Wafula, R. M. na Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: The Jomo Kenyata Foundation.

Wamitila, K.W. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia.* Nairobi: Focus Publications Ltd.

Wollstonecraft, M. (1792) *A Vindication of the Rights of Women*: W*ith Strictures on Moral andPolitical Subjects* (2nd ed.). London: J. Johnson. Inapatikana katika https://www.loc.gov/item/34033009/. Imesomwa tarehe 28/09/2023.